# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

# JARIDA LETU SONGEA MC

**YALIYOJIRI KUANZIA**

**APRILI 2023 HADI JUNI 2023**

## APRILI 2023 HADI JUNI 2023

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

**JARIDA LA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI MANISPAA YA SONGEA**

## DHIMA

**Kuhabarisha Umma taarifa mbalimbali za kiuchumi, za kijamii kutoka Idara na Vitengo na Taasis za Serikali Katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kuanzia mwezi Aprili hadi Juni 2023.**



**Mhe. Michael Mbano**
**Mstahiki Meya Manispaa ya Songea**



**Dkt. Frederick Sagamiko**
**Mkurugenzi Manispaa ya Songea**

## *YALIYOMO*

1. **Picha za miradi, na matukio mbalimbali ya kijamii, Siasa, na kiuchumi.**
2. **Makala mbalimbali.**
3. **Habari Maelezo.**

## RUHILA ZOO YAPOKEA SIMBA JIKE WAWILI KUONGEZA THAMANI YA UTALII

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori TAWA imeleta Simba wawili jike katika Bustani ya Ruhila Wildlife ZOO kwa lengo la kuhamasisha wananchi waweze kuwa na utalii wa ndani ambao ni utekelezaji wa Mkakati wa kuleta maendelezo katika ngazi ya Halmashauri, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Katika kuunga mkono jitihada za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Royal Tour ambayo imewezesha kuamsha amasa kubwa kwa Nchi kwa kuweka mkazo juu ya masuala ya Utalii ambayo husaidia kuleta mapinduzi katika Sekta ya utalii.

Katika kipindi cha miaka miatu 3 mfululizo Bustani ya Ruhila ZOO imeendelea kupata wageni mbalimbali ambao wamewezesha kuleta ongezeko la mapato ambapo kwa mwaka 2020/2021 walipata idadi ya watalii 252, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 walipata jumla ya watalii 724 na pia katika kipindi cha mwaka 2022/2023 julai hadi Februari walipata watalii 741.



Akizungumza Mkuu wa Wilaya ya Songea Kapenjama Ndile kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ambapo amewataka wananchi na viongozi wote kuwa na uzalendo katika kuhifadhi Bustani ya wanyama Pori kwa kuilinda, kuitunza kwa faida ya vizazi vijavyo kwa lengo la kukuza utalii na kuendeleza Uhifadhi wa Wanyama ambapo alisema kwa yeyote atakaye hujumu hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake." ***Alisisitiza***

Ndile amewataka wananchi kutembelea Bustani ili kujionea aina mbalimbali ya wanyama wakiwemo Simba, Pofu, Swala, Tembo, Pundamilia, Fisimaji, Digidigi pamoja na nyani wa njano.




Kwa upande wake Mstahiki Meya Manispaa ya Songea Michael Mbano alisema Nanukuu" Manispaa ya Songea ina vivutio vingi vya Utalii ikiwemo na Mlima Matogoro, Makumbusho ya Mashujaa ya Vita vya majimaji, pamoja na Ruhila ZOO ambayo leo tarehe 06 April imepokea Simba wawili 2 jike waitwao LUCY na Riana ambapo kupitia vivutio hivyo Manispaa ya Songea inaweza kuanzisha ***CITY TOUR, " mwisho wa kunukuu. Mbano alibainisha.***



Kamishina Msaidizi Kanda ya Kusini Mashariki TAWA Said Diwani Mshana alisema Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori imeendelea kujenga mabanda mbalimbali ikiwemo a banda la chui ambalo linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 15 April 2023 ambalo litatumika kwa ajili ya kuweka wanyama aina ya chui kwa lengo la kuongeza thamani ya Busatani ya Ruhila.

# UJIO WA MWENGE WA UHURU TAREHE 20/04/2023

Mkuu wa Wilaya ya Songea Kapenjama Ndile amewataka viongozi na wataalamu kushirki kikamilifu siku ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru ambao unatarajia kuwasili Manispaa ya Songea tarehe 20/04/2023 ukitokea **Halmshauri** ya Wilaya ya Madaba na utakabiziwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea katika kijiji cha Uyahudini tarehe 21/04/2023.



Agizo hilo limetolewa l kwenye kikao kazi cha Mkuu wa Wilaya ya Songea katika kikao cha Watumishi wa Manispaa ya Songea kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Songea tarehe 16 Aprili 2023 kwa lengo la kuratibu utekelezaji wa Mbio za Mwenge wa uhuru ambao utatembelea miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kauli mbiu ya mwaka 2023

"***Tunza Mazingira,Okoa vyanzo vya maji,kwa Ustawi wa Viumbe Hai na Uchumi wa Taifa"***

# MWENGE WA UHURU WARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MIRADI MAENDELEO



Mbio za Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa mwaka 2023 imepitia miradi 10 yenye thamini ya **shilingi 2,727,619,229.18** kati ya fedha hizo michango ya wananchi **shilingi 2,000,000.00**, Serikali Kuu **shilingi 1,447,715,329.18,** Wadau/Wahisani/Mtu binafsi wa maendeleo **shilingi 1,264,903,900.00** na Halmashauri ni **shilingi 13,000,000.00** ambapo kati ya hiyo 4 imefunguliwa, 1 umezinduliwa, 1 ni ugawaji wa vyandarua na 4 imetembelewa.



Ndugu Abdalla Shaibu Kaim Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa amezitaka Halmashauri zote Nchini zihakikishe zinaandaa miche ya miti zaidi ya 500 ambayo itapandwa ili kulinda na kutekeleza kwa vitendo ujumbe wa Mwenge wa Uhuru kwa lengo la kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanatunzwa na kusimamiwa vizuri kwa ustawi wa viumbe hai na Taifa kwa ujumla.

Kauli Mbiu ya Mwenge wa Uhuru 2023; "**MABADILIKO YA TABIA NCHI, HIFADHI YA MAZINGIRA NA UTUNZAJI WA VYANZO VYA MAJI, chini ya kauli Mbiu; Tunza Mazingira, Okoa vyanzo vya Maji kwa ustawi wa viumbe hai na Uchumi wa Taifa''.**

# MKUU WA MKOA WA RUVUMA KANAL. LABAN THOMAS AMEWATAKA WANANCHI KULINDA MUUNGANO.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban.Thomas amekemea vikali ndoa ya jinsia moja kwa vijana ambayo ni uvunjifu wa Mila na Desturi za Afrika.

Amewataka Wanafunzi kusoma kwa bidii ili waweze kupata mafanikio na kwa kupitia Elimu watakayoipata itawasaidia kusimamia Muungano na kutambua faida au manufaa ya Muungano.

Hayo yamejili wakati wa Maadhimisho ya Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao uliadhimishwa **kwa** kufanya ziara ya **kutembelea** miradi maendeleo na kuweka jiwe la Msingi la ufunguzi wa madarasa mawili ya awali yaliyojengwa kwa thamani ya shilingi Mil.43,160,000 fedha kutoka mfuko wa LANES 2021/202, uzinduzi wa Bweni la wasichana katika shule ya Sekondari Chabruma iliyojengwa kwa thamani ya Milioni 110 fedha kutoka Serikali kuu pamoja na upandaji wa miti kwenye maeneo ya shule kwa lengo la kuenzi Muungano wetu.



Kanal. Laban ametoa rai kwa wanachi wote kupanda miti ya vivuli, matunda ili kulinda na kutunza mazingira na kuboresha uoto wa asili na mazingira na kuimarisha vyanzo vya maji .

Naye Afisa Misitu Manispaa ya Songea Godfrey Luhimbo alisema Manispaa ya Songea inaendelea na mkakati wa kupanda miti ambapo siku ya sherehe ya Muungano ilipandwa miche 3000 na kufanya jumla ya miche imepandwa miche Mil.1,134,512 iliyofanikiwa kupandwa ndani ya mwaka 2023 kupitia Taasis za Serikali na za watu binafsi. ***Alibainisha.***



***Kwa upande wake wanafunzi kutoka shule tofauti zilizotembelewa na Kiongozi huyo ambapo wametoa shukrani zao kwa Serikali ya awamu ya sita kwa kuwawezesha kupata miundombinu ya bora ya elimu.***

# WANANCHI WAJITOKEZA KUFANYA USAFI KATIKA WIKI YA MAADHIMISHO YA MIAKA 59

Manispaa ya Songea imekuwa ikiendelea na utekelezaji wa WIKI ya Maadhimisho ya sherehe za miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kufanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo na upandaji wa Miti katika maeneo ya shule, kongamano mbalimbali za vijana na wazee, kukagua miradi, **Bonanza** la **michezo** na Usafi wa Mazingira katika maeneo ya kijamii na makazi.

Katika kutekeleza shughuli hizo Manispaa ya Songea imehitimisha Maadhimisho hayo leo tarehe 29 Aprili 2023 kwa kufanya usafi wa mazingira katika eneo la Soko la Bombambili kwa lengo la kuunga Mkono Maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na pamoja na kuweka mji katika mazingira ya Usafi.



Akizungumza Afisa Taka Ngumu na Usafi wa Mazingira Beno Philipo Mpwesa amewataka Viongozi wa Serikali za Mitaa, pamoja na Viongozi wa Masoko yote wahakikishe wanasimamia usafi wa Mazingira na kufanya ukaguzi wa nyumba hadi nyumba pamoja na kutumia sheria ndogo za usafi wa mazingira ambazo hutumika kwa yeyote atakaye vunja sheria ndogo hizo.

Beno aliongeza kuwa usafi wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi hivyo ametoa rai kwa jamii kushiriki kufanya usafi hususani usafi wa mwisho wa mwezi ambao hufanyika kila ifikapo mwishoni mwa mwezi husika.



Kwa upande wao wananchi wakizungumza na chanzo hiki cha Habari wametoa maoni yao kuwa **“ Muungano uendelee kudumishwa kwasababu unaleta Mshikamano, Umoja, Upendo na Amani ambao unasaidia watu kuishi kwa kusaidia na kushirikiana katika shughuli za kijamii hususani kushiriki kufanya Usafi wa Mazinngira.”** Mwisho wa kunukuu.

# ALAT RUVUMA YAFANYA ZIARA YA KUKAGUA MIRADI SONGEA DC



Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Ruvuma Mhe. Kelvin Mapunda amewataka Viongozi na Wataalamu Mkoani Ruvuma kuhakikisha wanasimamia zoezi la utoaji wa chakula kwa wanafunzi shuleni.

Akizungumza na wazazi wa shule ya Msingi Maleta iliyopo kata ya Ndongosi wakati wa Ziara ya kamati ya ALAT ( Jumuiya ya Tawala za **Serikali** za Mitaa Tanzania) kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi maendeleo ya Halamshauri ya Wilaya ya Songea.

Amepongeza wananchi wa kitongoji cha Maleta kwa kuweka Mkakati **rafiki** ambao unatekelezeka na wananchi hao kwa kuwa na mwitikio mkubwa wautoaji wa chakula kwa wanafunzi 327 wakiwemo wavulana 160 na wasichana 167. ***"Aliwapongeza".***

Mhe, Mapunda amesema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka Mpango Mkakati wa kuondoa changamoto ya uhaba wa miundombinu ya shule kwa shule za Msingi Mwl Maghembe ametoa shukrani kwa Serikali ya awamu ya sita kwa kuwapatia fedha zaidi ya Bil 2 kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya ikiwa ni miongoni mwa Halmashauri 8 Kitaifa zilizopewa fedha kwa ajili kujenga jengo la Wagonjwa wa TB na Ukoma**.**



**Shule ya Msingi Maleta ipo katika kijiji cha Ndongosi katika kata ya Ndongosi ambayo ilianza kama shule shikizi yenye jumla ya wananfunzi 327.** kupitia mradi wa BOOST ambao utaanza kutekelezwa hivi karibuni.



Amewataka wananchi kuendelea kuwa na uzalendo wa kuchangia nguvu za wananchi wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kitongoji hicho.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mwl. Neema Maghembe alisema " Ziara ya kamati ya ALAT Mkoa wa Ruvuma ilianza kwa kutembelea miradi ya maendeleo ikiwemo na ujenzi wa madarasa **mawili** na ofisi ya walimu shule ya Msingi Maleta "Shikizi" ambayo iliyojengwa kwa gharama ya shilingi Mil. 40 ikiwa nguvu za wananchi ni shilingi 3,260.000, Mfuko wa Jimbo tsh 2,000,000, ofisi ya Mkurugenzi kiasi cha Mil 16,000,000 fedha za mapato ya ndani pamoja na vifaa vya ujenzi.

# YALIYOJIRI MEI MOS 2023

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban Thomas amewataka watumishi wa Umma Mkoani Ruvuma kuacha tabia ya Uchonganishi maofisini ambayo hupelekea kuleta **migogoro** baina ya Watumishi na kuathiri utendaji wa kazi.

Kauli hiyo imetolewa kwenye maadhimisho ya Mei Mos ya Kimataifa ambayo huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 01 Mei ambayo Kimkoa imefanyika katika Uwanja wa Majimaji Mjini Songea.

Kanal. Laban amewataka waajiri wote kutatua changamoto zilizo chini ya uwezo wao ikiwemo na malipo ya nauli za likizo, malipo ya posho za wajumbe wa baraza la wafanyakazi na stahiki mbalimbali za madai ya watumishi wa umma.

Ametoa rai kwa waajiri wa Taasis zisizo za kiserikali kuhakikisha wanawaruhusu watumishi wao waweze kujiunga kwenye vyama vya wafanyakazi ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria .



Amesema Sambamba na utekelezaji majukumu ya kiutumishi Serikali ya awamu ya Sita inaendelea na mikakati ya kuboresha miundombinu ya elimu msingi kupitia mradi wa BOOST ambapo kwa Mkoa wa Ruvuma imepokea zaidi ya Bil. 7 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule za msingi.




Naye Mwenyekiti wa TALGWU Mkoa wa Ruvuma Willey Luambano amesema anatoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa kutatua baadhi ya changamoto za watumishi ikiwemo na kupandisha madaraja kwa watumishi.

Willy aliongeza kuwa kupitia ajira mpya zilizotolewa na Serikali hivi karibuni zitawezesha kuongeza wanachama wapya ambapo TALGWU imsajili jumla ya wanachama 3229 kati ya hao watumishi wanachama walioteuliwa kupakea ufanyakazi Bora ni 106.

KAULI MBIU YA MWAKA 2023; ***MISHAHARA BORA NA AJIRA ZA STAHA NI NGUZO KWA MAENDELEO YA WAFANYAKAZI WAKATI NI SASA..***

# Yaliyojiri wakati wa mazishi ya aliyekuwa diwani kata ya mfaranyaki

Manispaa ya Songea imejaa Simanzi na Masikitiko makubwa baada ya kutokea kifo cha Mhe. Ajira Rajbu Kalinga aliyekuwa Diwani wa kata ya Mfaranyaki ambaye amefariki Dunia tarehe 06 Mei 2023 katika Hosptali ya BO-CHI Jijini Dar es salaam alipokuwa akipatiwa matibabu na kuzikwa tarehe 08 Mei 2023 katika Makaburi ya Mfaranyaki Manispaa ya Songea.

Marehemu Mhe. Ajira Kalinga aliwahi kutumikia nafasi ya Udiwani wa Viti Maalmu katika kipindi cha mwaka 2018-2020 pia kupitia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 Marehemu alifanikiwa kugombea nafasi ya Udiwani ambao alishinda katika kata ya Mfaranyaki.

Mstahiki Meya Manispaa ya Songea Michael Mbano alisema **" Enzi za Uhai wake Mhe. Ajira Kalinga alikuwa Mpiganaji na mpambanaji katika kuwahudumia wananchi wake katika kuleta maendeleo katika kata yake hivyo hamna budi kuyatekeleza mema yote ambayo Marehemu Ajira alianza kuyatekeleza**." alisisitiza.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Songea Wilman Kapenjama Ndile alisema " Marehemu Ajira Kalinga alimfahamu kwa utendaji wake wa kazi uliotukuka ambapo mara ya kwanza alimfahamu akiwa ana siku mbili tangu aanze kazi na mara baada ya kumtembelea ofisini kwake ambapo aliweza kumshirikisha changamoto mbalimbali zinazohusu miundombinu ya shule za msingi na Sekondari katika kata ya Mfaranyaki."

Ndile amewataka wananchi na Viongozi wote kuendelea kuyaenzi mema na mazuri yote ambayo Marehemu Ajira Kalinga alikuwa ameanza kuyatekeleza pamoja na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kumpa pumziko la milele. Amina.

Kwa upande wake Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (MB) Waziri wa Katiba na Sheria alitoa salamu za pole kwa familia, wananchi wa Manispaa na CCM, kutoka kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutokea kifo cha aliyekuwa Diwani wa kata ya Mfaranyaki Mhe. Ajira Kalinga.

Dkt. Ndumbaro alisema Kwa masikitiko na huzuni kubwa Chama kimepoteza Kiongozi mahiri, Mpiganaji, Mtetezi wa wananchi, hivyo hatuna budi kumuombea apumzike amani**." Alihuzunika**"

Alisisitiza wakati tunaombeleza tutafakari mema mazuri ambayo marehemu aliyaanza kuyatekeleza na baadhi yake yataanza kutelezwa hivi karibuni ikiwemo na barabara kiwango cha Lami.

Naye kwa upande wake Komredi Oddo Mwisho Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi amewataka Wenyeviti wa Mitaa, Watendaji wa kata kuhakikisha wanasimamia na kuendeleza shughuli zote zilizokuwa zikitekelezwa na Marehemu Mhe. Ajira Kalinga.

Innalillahi wanailillahi Raijun.

# ZIARA YA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI ILIVYOTEMBELEA-MIRADI YA MAENDELEO.



KAMATI ya Fedha na Uongozi Manispaa ya Songea ikiongozwa na Mstahiki Meya Michael Mbano amewataka wataalamu kuhakikisha wanasimamia miradi kikamilifu na kukamilika kabla tarehe 30 juni 2023.

Agizo hilo limetolewa katika ziara ya **kamati** ya Fedha na Uongozi iliofanyika kwa siku mbili kuanzia tarehe 11 hadi tarehe 12 Mei 2023 kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo ili kulinganisha hali ya mradi na thamani ya fedha.



Miongoni mwa miradi iliyotembelewa ni pamoja na mradi wa ukamilishaji wa chumba 1 cha darasa shule ya Msingi Ruvuma kwa thamani ya Mil. 18,750,000 fedha kutoka Serikali kuu, ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 2 Shule ya Msingi Mbulani kwa thamani ya Mil. 25,000,000 kutoka Serikali kuu, Ukamilishaji wa Madarasa 2 Shule ya Msingi Kipera kwa thamani ya Mil. 20,000,000 fedha za mapato ya ndani, na Ujenzi wa Uzio.

Bweni la watoto wenye mahitaji maalumu Shule ya Msingi Subira kwa thamani ya Mil. 60, 000,000 fedha ktoka Serikali kuuMiradi mingine ambayo imetembelewa ni pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Mtaa wa LAMI kwa thamani ya Mil. 15,000,000 fedha kutoka mapato ya ndani, ukamilishaji wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Muungano kwa thamani ya Mil. 5,000,000 fedha kutoka mapato ya ndani, Ukamilishaji wa madarasa mawili 2 Shule ya Msingi Londoni kwa thamani ya Mil. 25,000,000 kutoka Serikali kuu, Ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Msingi London kwa thamani ya Mil. 20,000,000 fedha kutoka mapato ya ndani, na ukamilishaji wa bweni 1 la Shule ya Sekondari ya Wavulana kwa thamani ya Mil. 22,000,000 fedha kutoka Serikali kuu.

Aidha Miradi mingine ni ukamilishaji wa matundu 10 ya vyoo shule ya Msingi Likuyufusi kwa thamani ya Mil. 10,000,000 fedha kutoka Serikali kuu, ukamilishaji wa madarasa mawili Shule ya Msingi Sabasaba kwa thamani ya Mil. 25,000,000 fedha kutoka Serikali kuu, Ukamilishaji wa Maabara Shule ya Sekondari Matarawe kwa thamani ya Mil. 12,000,000 fedha za mapato ya ndani, pamoja na ukarabati wa Ofisi ya Kata ya Matarawe kwa thamani ya Mil 5,000,000 fedha za mapato ya ndani.

# SIKU YA WAUGUZI DUNIANI




Siku ya wauguzi Duniani ( International Nurse Day) huadhimishwa ulimwenguni kote kila mwaka tarehe 12 Mei wakikumbuka na kutafakari mchango wao wanaotoa kwa jamii.

Siku hiyo iliibuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1953 na Dorothy Sutherland aliyekuwa Afisa kutoka kitengo cha Elimu ya Afya na Ustawi Nchini U.S kwa lengo la kuangalia mchango wa Wauguzi katika kuhudumu jamii.

Baraza la Wauguzi Ulimwenguni (International Council of Nurse) ilianza kuadhimisha siku hiyo tangu mwaka 1965 na mwaka 1974 Januari ambapo ilitolewa tamko rasmi kuwa Siku ya Wauguzi Duniani iadhimishwa Ulimwenguni kote tarehe 12 Mei.Hayo yalibainishwa kwenye sherehe za maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani iliyofanyika kiwilaya katika Viwanja vya Mjimwema Kituo cha Afya na kuhudhuriwa na Wauguzi, pamoja na wadau mbalimbali wa afya.

Akizungumza Afisa Elimu Manispaa ya Songea Mwl. Janeth Moyo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea alisema Chama cha Wauguzi Tanzania Tawi la Manispaa ya Songea kinaendelea na jitihada za makusudi za kukemea wauguzi wanaofanya kazi kinyume na makubaliano, kanuni na Sheria za kazi ya uuguzi, wauguzi kwani sio wauguzi wote ambao si waadilifu kwa wagonjwa n a jamii kwa ujumla. **Alibainisha.**



Aliongeza kuwa Serikali inaendelea na mikakati ya kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ya kazi ya muuguzi pamoja na kuwawezesha wauguzi kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya Taaluma na maadhimisho ya kimataifa ya siku ya Wauguzi pamoja na kuajiri watumishi wa ajira mpya**.**




Kwa upande wake Muuguzi Mkuu Manispaa ya Songea Theodosia Ngowoko alisema Kauli Mbiu ya mwaka 2023 isemayo "WAUGUZI MUSTAKABALI WA AFYA YETU" OUR NURSES OUR FUTURE" Kauli mbiu hiyo inaangazia umuhimu wa kuwalinda Wauguzi, kuwekeza katika fani ya uuguzi na kuheshimu haki za Wauguzi kwa kujenga mifumo thabiti ya Afya ya hali ya juu ili kukidhi mahitaji ya jamii.

Ngowoko aliongeza kuwa kuelekea kilele cha maadhimisho hayo shughuli mbalimbali za kijamii bila malipo zilifanyika ikiwemo na upimaji wa VVU, Huduma ya Uzazi wa Mpango, Uchunguzi wa Saratani ya Mlango wa kizazi, Kutoa huduma ya Tohara, ambapo shughuli hizo zilianza kuadhimishwa kuanzia tarehe 10 Mei 2023 hadi siku ya kilele tarehe 12 Mei 2023. ***Alibainisha.***

# RC RUVUMA " AMEWATAKA WAZAZI KUZINGATIA MALEZI BORA KATIKA NGAZI YA FAMILIA"

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban Thomas amewataka wazazi kudumisha upendo na mshikamano ndani ya familia ili kujenga malezi bora katika jamii.

Niwajibu wa kila mzazi kujikita katika usimamizi wa malezi ambayo ni msingi ikiwemo na kumjali mtoto katika mahitaji yake ya msingi , kumlinda mtoto dhidi ya ukatili pamoja na kuzungumza na mtoto mara kwa mara ili kujua changamoto **zinazomkabili** na maendeleo yake.



Hayo yamejili katika mahadhimisho ya siku ya familia duniani , ambayo hufanyika kila ifikapo Mei 15 kila mwaka, ambayo kimkoa yamefanyika katika Bustani ya Manispaa ya Songea na kuhudhuliwa na wataalamu mbalimbali, wakiwemo na wadau, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa wadini pamoja na wananchi mbalimbali kwa lengo la kukumbusha jamii juu ya umuhimu wa malezi bora ngazi ya Familia.



Kanal. Laban amesema **" Mustakabali wa malezi bora ya watoto yanatakiwa kusimamiwa na wazazi au walezi kwa kuzingatia maadili mema ili kuepusha migogoro ambayo yanaweza kusababisha familia kusambaratika na kuacha watoto bila uangalizi mzuri ambayo hupelekea watoto kukosa huduma muhimu"**. ***Alisistiza***.

# KATA YA MATOGORO YAKABIDHI MADAWATI 502 KUTATUA CHANGAMOTO ZA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI



Kata ya Matogoro nimiongoni mwa kata 21 zilizopo ndani ya Manispaa ya Songea ambayo imekuwa ikitekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kushirikisha wananchi na Wadau katika kutatua changamoto za miundombinu ya Elimu, Afya kwa lengo kuunga Mkono Jitihada za Serikali ya awamu ya sita Katika kutatua changamoto hizo kwa kushirikiana na wataalamu, wananchi na uongozi wa kata wameweza kutengeneza Madawati **302 kwa kupitia nguvu za wananchi, na madawati 120** mchango kutoka kwa Mhe. Diwani sawa na jumla ya **madawati 502** kwa ajili ya shule Sekondari na Shule ya Msingi Matogoro.

Hayo yamejili wakati wa kukabidhi madawati kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea iliyofanyika kwenye mkutano wa hadhara ambao ulihudhuriwa na wananchi, viongozi wa vyama vya Siasa, Wataalamu na Wanafunzi katika Shule ya Sekondari Matogoro tarehe 17 Mei 2023.

Akipokea madawati hayo Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Dkt. Frederick Sagamiko alisema " Niwa jibu wa Serikali kuhakikisha wanafunzi wanapata miundombinu bora ya kusomea na kijifunzia ikiwemo na madawati, viti, meza na madarasa ambapo katika kutekeleza wajibu Serikali ilitoa fedha Bil 1.52 kujenga madarasa 76 na madawati 3800 ili kuboresha mazingira ya Elimu.

Akitoa pongezi kwa Uongozi wa Kata ya Matogoro kwa uzalendo uliotukuka kwa kutengeneza madawati/Viti na Meza 502 kwa lengo la kuondoa upungufu wa madawati kwa wanafunzi, utoaji wa chakula shuleni nauanzishaji wa Benk ya madawati. ***"Aliwapongeza***."

Dkt. Sagamiko aliongeza kuwa, Diwani wa kata ya Matogoro ni kiongozi mwenye mfano wa kuigwa kwa kuwa hupenda kushirikisha jamii yake anayoitawala katika kutanzua changamoto za kata yake bila kusubili mchango kutoka Halmashauri.



**Amewataka** Watendaji wa kata nyingine kuja kujifunza namna wanavyo fanikiwa katika utendaji wa kazi hususani usimamiaji bora wa miradi na kukamilisha ujenzi wa miradi kwa wakati. ***"Alibainisha na kusisitiza."***

*Inaendelea*

Kwa upande wake Diwani wa kata ya Matogoro Issa Mkwawa alisema “ Kutokana na upungufu uli-ojitokeza wakati anaingia madarakani, waliandaa Mpango Mkakati wa kuweka Benk ya Madawati kwa ajili ya Shule za Msingi na Shule za Sekondari ili kuondoa tatizo la upungufu wa madawati ambao hadi kufikia tarehe 17 Mei 2023 wameweza kutengeneza madawati 502 ambayo yamekabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea. “***Aliwashukuru”.***



Naye Afisa Elimu kata ya Matogoro Samson Mbunda alisema Shule ya Sekondari Matogoro ina jumla ya wanafunzi 1080, na shule ya Msingi Matogoro ina jumla ya Wanafunzi 1032 ambapo kutokana na ushirikiano kutoka kwa wananchi, pamoja na Diwani wa Kata hiyo wameweza kutengeneza viti 502 ambayo yamekabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea kwa ajili ya matumizi ya shule husika hivyo kwasasa hakuna upungufu wowote wamadawati.

# TAKUKURU RUVUMA YAFUATILIA ZAIDI YA BIL. 6 FEDHA ZA MRADI.



TAKUKURU Mkoani Ruvuma imefanikiwa kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Bil. 6 ambayo imekutwa na mapungufu mbalimbali ikiwemo na miradi kutokamilika kwa wakati, ununuzi wa vifaa vichache, na ucheleweshaji wa malipo ya Mafundi.

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo, Miradi mitano yenye thamani ya shilingi 5,510,000,000 ilikuwa na mapungufu ikiwemo na mradi wa ujenzi wa Madarasa 9 katika Shule ya Sekondari Sasawala Wilaya ya Namtumbo kwa thamani ya 180,000,000, Ujenzi wa majengo Matatu katika Hosptali ya Wilaya ya Namtumbo kwa thamani ya 800,000,000, jengo la wagonjwa wan je katika Hosptali ya Rufaa Mkoa Songea kwa thamani ya 3,870,000,000, ujenzi wa Hosptal ya Wilaya ya Mbinga 500,000,000 pamoja na kituo cha afya Mbangamao 250,000,000.

Hayo yamejili katika kikao cha Waandishi wa Habari kilichofanyika leo 18 Mei 2023 katika ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kuuhabarisha umma kuhusu utendaji kazi wa ofisi ya TAKUKURU katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi januari hadi machi 2023.

Akitoa ***ufafanuzi*** Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma Janeth Haule alisema “ **miongoni** mwa mikakati itakayotekelezwa katika kipindi cha miezi mitatu ijayo ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya Rushwa na madhara yake katika usimamizi wa miradi ya maendeleo, kuendelea kufanya kazi za kuzuiia na kuchukua hatua kwa wale wote watakao kutwa na tuhuma za vitendo vya Rushwa ikiwa ni pamoja na kwafikisha Mahakamani, kufanya uchunguzi na kuchukua hatua kwa watakao kutwa na tuhuma za vitendo vya Rushwa, na kushirikiana vijana wa Skauti katika kutoa elimu ya mapambano dhidi ya Rushwa pamoja na Program Rafiki.

Janeth ametoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano na TAKUKURU kwa taarifa zenye kuashiria vitendo vya Rushwa.

# VISHIKWAMBI 50 VYATOLEWA KWA MADIWANI, WAKUU WA IDARA NA VITENGO



Halmashauri ya Manispaa ya Songea kupitia Baraza la Madiwani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 **liliidhinisha** Bajeti pamoja na kuadhimia kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha kununa **VISHIKWAMBI** kwa ajili ya matumizi ya Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo katika uendeshaji wa shughuli za vikao vya Menejimenti, Vikao vya Halmashauri pamoja na vikao vya Baraza la Madiwani ili kupunguza matumizi ya karatasi.

HATUA hiyo imetekelezwa kwa asilimia 100% ambapo Halmashauri imeweza kununa na kugawa Vishikwambi 50 vyenye thamani ya zaidi ya Mil. 20 kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa Rasilimali za Umma.

Zoezi hilo limefanyika jana tarehe 17 Mei 2023 katika ukumbi wa Manispaa ya Songea lililoendana na utaoaji wa Mafunzo elekezi ya matumizi sahihi ya mfumo wa TEHAMA na utunzaji wa nyaraka za Serikali yalihudhuriwa na Madiwani, Viongozi ngazi ya Wilaya na Wakuu wa Idara.

Mstahiki Meya Manispaa ya Songea Michael Mbano alisema " Vishikwambi vitasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa Taasis, uhakika wa upatikanaji wa taarifa, pamoja na urahisishaji wa utendaji wa kazikwa haraka. **Alipongeza.**



Mhe. Mbano amewataka Waheshimiwa Madiwani kuzingatia kanuni na taratibu za utunzaji wa siri wa nyaraka za Serikali pamoja na kifaa chenyewe ili mara baada ya kukoma madaraka ya uongozi kila aliyepewa kishikwambi atatakiwa kukikabidhi mikononi mwa Serikali. " Mbano **amesisitiza.** "

Mkurugenzi Manispaa ya Songea Dkt. Frederick Sagamiko alisema " Katika kutekeleza agizo hilo Manispaa ya Songea imenunua Vishikwambi 50 na kuvikabidhi kwa Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kuachana na matumizi ya karatasi na kwenda Digital ( Serikali Mtandao). DKT. Sagamiko "**Alisisitiza"**.



*Inaendelea*

**Kwa upande wake Afisa TEHAMA Manispaa ya Songea Mvano Mbalale alisema Mafanikio ya TEHAMA yatawezesha ongezeko la mapato ya serikali, kupunguza gharama vikao kupitia mikutano ya kimtandao, nakupunguza gharama za uendeshaji wa vikao kwa kutumia vifaa vya TEHAMA vinavyotumia nyaraka laini badala ya nyaraka ngumu ili kulinda na miundombinu ya nyaraka za Tehama, Serikali imeandaa Sera na Miongozo ya Usimamizi ambayo ipo kisheria ukiukwaji wa Miongozo hiyo ni Uvunjivu wa Sheria.**

**Mvano alisema Miongoni wa Sera hizo ni pamoja na Sera ya Tehama (ICT policy), Sera ya kwa Mtumiaji wa Tehama(ICT use Acceptable Policy) Sera ya Ulinzi (ICT security Policy) na Mwongozo wa Matumizi Bora Sahihi na Salama Mifumo na Miundombinu ya Tehama. "*Alibainisha*"**



***isha.***

**Wakizungumza kwa nyakati tofauti waheshimiwa Madiwani hao ambapo walianza kwa kuipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha kanuni na sheria na miongozo ya Matumizi sahihi ya TEHAMA ambayo inazitaka Taasis kutumia Vishikwambi na kuachana na Matumizi ya karatasi kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa rasilimali za umma na upotevu wa nyaraka. " *Walishukuru.* "**

# ZIARA YA MADIWANI KUTOKA IRINGA MC, WALIVYOTEMBELEA MACHINJIO YA KISASA SONGEA MC

Manispaa ya Songea inaeendelea kupokea wageni kutoka nje Mkoa wa Ruvuma wakifika katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu katika utekelezaji na usimamizi wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kwa mara nyingine tarehe 22 Mei 2023 Manispaa ya Songea ilipokea Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ambao walikuja kwa lengo la kujifunza namna inavyoendeshlatowa na kusimamia machinjio ya kisasa ya Songea ikiwemo na tozo, na kiutawala.

Akizungumza Mstahiki Meya Manispaa ya Iringa Ibrahimu Ngwada alisema **Manispaa** ya Iringa ina machinjio ambayo bado haijakamilka japokuwa imeanza kufanya kazi na huchinja katika mfumo ambao sio wa kisasa.



Mhe. Ngwada alisema kupitia hilo walipendekeza kuja Manispaa ya Songea ili kuboresha utendaji wa kazi pia kuendelea kuweka mahusiano ya ki-Halmashauri hasa ikiwa inaendesha miradi inayofanana ni muhimu ujifunze kupitia wengine

Naye Mkurugenzi Manispaa ya Songea Dkt. Frederick Sagamiko alianza kwa kuwakaribisha wageni kisha alieleza Mradi huo umegharimu kiasi cha Bil. 5.7 na umeanza kutoa huduma japokuwa bado haujakamilika kwa asilimia 100%.



Alisema kuwa **mfumo wa uchinjaji nyama katika machinjio hiyo ni wa kisasa ambao unatumia mtambo ambapo Manispaa ya Songea ni miongoni mwa miji michache nchini Tanzania ambayo inatumia mtambo huo**.

Dkt. Sagamiko aliongeza kuwa **kupitia machinjio ya kisasa mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea yameongezeka ambapo** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 walikisia kukusanya kiasi cha Mil 379.

# BARAZA LA MADIWANI LATOA AGIZO UTOAJI WA CHAKULA SHULENI.



Mstahiki Meya Manispaa ya Songea Michael Mbano amewataka Wataalamu wote kuhakikisha wanatoa ushirikiano katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kuikamilisha kwa wakati kabla ya tarehe 30 juni 2023.

Amesema kila kiongozi anatakiwa kuwajibika katika eneo lake kwa kuishirikisha jamii husika ili kutatua changamoto za wananchi ikiwemo na miundombinu ya shule, Afya na Barabara kwa lengo la kuunga mkono jitihada za Serikali ya awamu ya sita.

Alibainisha kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza Manispaa ya Songea ilipokea zaidi ya Bil. 1.5 pia katika kipindi cha robo ya pili na ya tatu Manispaa ya Songea imepokea Bil. 1.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. ***Alipongeza".***

Mhe. Mbano amewataka Madiwani wote kutembelea kata ya Matogoro kujifunza namna walivyoweza kufanikisha kutatua changamoto za madawati kwa shule za msingi na Sekondari kwa lengo la kuondoa changamoto mbalimbali za wananchi ". Alisisitiza."

Ametoa wito kwa wataalamu kuhakikisha wanaongeza bidii ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, utoaji wa chakula kwa wananfunzi shuleni, pamoja na usafi wa mazingira**." Mhe. Mbano alibainisha."**



Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Songea Mjini Komredi Mwinyi Msolomi amewataka Wataalamu kusimamia usafi wamazingira hususani katika maeneo ya Soko, na makazi ya watu.

Naye katibu wa CCM Wilaya ya Songea Mjini James Mgego ametoa wito kwa watumishi na Madiwani kuhakikisha wanasimamia miradi ya maendeleo na kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kufikia lengo lililokusudiwa na Serikali.

# SHULE ZOTE ZIHAKIKISHE ZINATOA CHAKULA CHENYE VIRUTUBISHO IFIKAPO JULAI 2023



Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Dkt. Frederick Sagamiko amewataka maafisa Elimu Msingi na Sekondari na maafisa lishe kuhakikisha wanasimamia zoezi la wanafunzi kupata chakula chenye viini lishe ili kuondoa hali ya udumavu.

Hayo yamejili katika kikao cha kamati ya lishe cha robo ya tatu ya mwaka ambacho kimefanyika tarehe 24 Mei katika ukumbi wa Manispaa ya Songea na **kuhudhuriwa** na viongozi wa dini, watalaamu pamoja na wadau mbalimbali kwa lengo la kufanya tathimini ya hali ya Lishe ngazi ya Halmashauri.

Dkt. Sagamiko ametoa rai kwa maafisa Watendaji kata/mitaa kushirikiana na maafisa lishe katika kuhamasisha na kuwaelimisha wazazi wajibu **na** umuhimu wa kuchangia chakula kwa wanafunzi shuleni katika kipindi cha masomo yao.



Kwa upande wake Mganga mkuu wa Manispaa ya Songea Dkt. Amos Mwenda amewataka maafisa lishe kufanya ukaguzi wa viwanda vya usindikaji wa chakula kuhakikisha vinakuwa na mashine za kuchanganyia viini lishe.

Alisema Wazabuni wanapaswa kupewa Elimu juu ya kusambaza chakula chenye virutubisho shuleni ili kujenga afya za wanafunzi na kuondoa tatizo la utapia mlo na udumavu katika jamii Manispaa ya Songea***. Dkt.Mwenda alibainisha***

Naye Afisa lishe Manispaa ya Songea Albert Sinkamba amewataka maafisa Elimu Msingi na Sekondari kutoa ushirikiano kwa maafisa watendaji kata/mitaa wakati wa kufanya vikao mbalimbali vya wananchi au wazazi na kutoa miongozo kwa wazazi juu ya mustakabali wa kuchangia chakula shuleni.

# NGO'S 37 ZA SHIRIKI KIKAO CHA TATHIMINI YA UTENDAJI KAZI WILAYA YA SONGEA.



Mkuu wa Wilaya ya Songea Mhe.Wilman Kapenjama Ndile amezitaka Asasi za kiraia kuhamasisha shughuli za maendeleo na kutoa huduma katika jamii ili kuondoa changamoto zinazowakabili.

Asasi za kiraia (NGO'S) ni chombo muhimu ambacho husaidia kufahamu na kutatua matatizo mbalimbali na kutoa huduma ikiwemo kutoa elimu ya uzazi wa mpango kwa jamii, mapambano dhidi ya Ukimwi na madawa ya kulevya, mapambano dhidi ya malaria, pamoja na kutoa huduma kwa watoto na wazee waishio mazingira hatarishi. ***Mhe. Ndile alisema.***

Akizungumza na mashirika yasiyo ya serikali (NGO'S) katika mkutano wa mwaka wa fedha 2021/2022 wilaya ya Songea ambao umefanyika Mei 25 katika ukumbi wa Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na viongozi wa dini, watalaamu pamoja na wadau kutoka asasi mbalimbali ambapo mkutano huo umeadhimisha utoaji wa huduma katika maeneo ambayo serikali hayajayafikia ili kuondoa mrundikano wa kero katika jamii.

Mhe. Ndile amezitaka asasi za kiraia kujisajili katika ofisi za maendeleo ya jamii katika halmashauri/ ofisi ya msajili ya mkuu wa wilaya ya Songea kwa kufuata taratibu na kanuni ziliwekwa ili zitambulike kisheria na zishirikishwe na serikali kwa kuzingatia miongozo husika

Kwa upande wake Afisa maendeleo ya jamii Manispaa ya Songea Martin Mtani ameyataka mashirika yasiyo ya serikali kuendelea kutoa elimu katika jamii juu ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja na kupinga vikali ndoa ya jinsia moja yakiwa na lengo la kuunga juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya sita ili kulinda na kuimarisha mila na desturi ya kitanzania.

Asasi za kiraia zilizoshiriki mkutano huo jumla 37 kiwilaya kati ya hizo 15 kutoka Manispaa ya Songea na 22 kutoka halmashauri ya Songea DC pamoja na halmashauri ya Madaba, **mafanikio yaliyopatikana kutokana na utendaji kazi mzuri wa asasi hizo yakiwemo kusaidia serikali kukusanya takwimu maalumu kwa ajili ya mipango ya maendeleo, kutoa elimu ya mafunzo ya kilimo pamoja na kuunganisha nguvu ya pamoja kati ya mashirika na serikali katika kuleta maendeleo katika jamii.** Mtani alisema

Tunatoa shukrani kwa sekretarieti ya wilaya ya Songea kwa kuanda mkutano huu ambao utoa miongozo namna ya kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia sheria zilizowekwa na serikali ili kuleta maendeleo katika wilaya ya Songea na Taifa kwa ujumla.***walishukuru***

# UTOAJI WA CHAKULA SHULENI NI LAZIMA " DC SONGEA ASISITIZA"



MKUU wa Wilaya ya Songea Wilaman Kapenjama Ndile amewataka Viongozi wa Serikali za Mitaa/kata kusoma taarifa ya mapato na matumizi kwa kila robo ya mwaka ili kuweka uwazi na uwajibikaji kwa wananchi wanaowaongoza.

Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, Ibara ya 145 na 146, Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi ambavyo vipo katika ngazi ya chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambavyo huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe ambapo huwezesha wananchi kuwa na Sauti katika maamuzi mbalimbali kwa kushiriki moja kwa moja au kupitia wawakilishi wao katika shughuli za maendeleo na utawala.

Kwa kuzingatia hilo Serikali ya Mtaa kupitia Mwenyekiti wa Mtaa inao wajibu kutoa taarifa za mbalimbali za maendeleo ya mtaa husika ikiwemo na kusoma mapato na matumizi ya fedha zilizopokelewa kupitia mkutano wa hadhara kwa lengo la kuweka uwazi na ushirikishwaji jamii na endapo hatatoa taarifa ya Mapato na Matumizi anaweza kushitakiwa kwa mujibu sheria.

Hayo yamejili katika kikao kazi cha Maafisa Watendaji wa Mitaa 95, Wenyeviti wa Mitaa 95, Watendaji wa kata 21, kamati ya Ulinzi na usalama, pamoja na Wakuu wa idara na Vitengo kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Songea tarehe 03 Mei 2023 kwa lengo la kuwakumbusha majukumu yao watendaji na wenyeviti wa mitaa katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Mhe. Ndile alisema Serikali ikitoa maagizo huna budi kutekelezwa hivyo amewataka Viongozi hao kuhakikisha wanasimamia suala la mzazi kuchangia chakula cha shule kwa shule za msingi na Sekondari ifikapo julai 2023 kwa lengo la kuinua ufaulu wa wanafunzi.

Aliongeza kuwa ili kufanikisha zoezi hilo kila mtaa unatakiwa kuitisha vikao vya kamati za



Serikali za Mtaa, mikutano ya hadhara, Bodi za shule pamoja na kamati za shule ili kuweka mkakati bora wa utekelezaji na usimamizi wa michango kutoka kwa wazazi ikiwemo na kufungua akaunti na utunzaji wa chakula.

Hali halisi ya utoaji wa chakula shuleni Wilaya ya Songea kwa Halmashauri ya Madaba ni 96%, Halmashauri ya Wilaya ya Songea ni 97% ana Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni 67%. ***Mhe. Ndile " Alibainisha."***

Kwa upande wake Afisa utumishi Manispaa ya Songea Sadiki Mrisho akiwakumbusha majukumu ya Wenyeviti na Maafisa watendaji wa mtaa aliserma Mwenyekiti wa Mtaa atakuwa Mwenyekiti wa mikutano yote ya kamati ya mtaa na Mkutano wa Hadhara, Msuluhishi wa migogoro midogomidogo ambayo haistahili kuitisha **mikutano** wa mtaa au kupeleka baraza la kata au Mahakama, kuwaongoza na kuwahimiza wakazi wa mtaa shughuli za maendeleo, kutekeleza kazi atakazopewa na kamati ya mtaa na Mkutano Mkuu wa Mtaa au kamati ya maendeleo ya kata na nyinginezo.

Aliongeza kuwa Wajibu wa Afisa Mtendaji wa Mtaa ni kuwa Mtendaji Mkuu wa Mtaa, kusimamia utekelezaji wa Sera za Halmashauri, kuishauri kamati ya maendeleo ya Mtaa kuhusu maendeleo ya Mtaa, kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo pamoja na sheria nyingine, kuishauri kamati ya mtaa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama na nyinginezo. **"Mrisho**




**alibainisha."**

Kwa upande wake OCD Songea S.S.P Wilbert Mila Siwa alisema jeshi la Polisi limeundwa kwa mujibu wa ibara ya 147 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayyo imebainisha wajibu wa Serikali ndani ya majeshi ya ulinzi na usalama wa wananchi wa Tanzania ambayo ni pamoja sheria ya polisi na Polisi wasaidizi Sura 322 kifungu cha 5 imesema kuhakikusha uwepo wa amani na usalama, kuzuia makosa ya uhalifu kabla hayajatendeka, kulinda maisha na mali za Watanzania, kusimamia sheria na kanuni za nchi, kukamata wahalifu na kupeleeza pamoja na kudhibiti makosa ya usalama barabarani.

S.S.P Siwa alisema Jeshi la Polisi limejikita katika mambo makuu matatu katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao ikiwemo na Weledi, Usasa, na Ushirikishwaji wa jamii. **Alibainisha"**

Kwa upande wake Inspekta wa Jeshi la Polisi Songea Melinda Mgumba kutoka Dawati la jinsia na watoto ni sehemu maalmu katika kituo cha Polisi inayoshughulikia Waaathirika wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na watoto kwa lengo la kutenganisha sehemu ya huduma kwa waathirika wa ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, kumpa muathirika nafasi ya kutulia itakayomfaa ili asiendelee kudhalilika, kusikiliza maelekezo kwa usiri mkubwa, kutoa ushauri kutegemea na lalamiko lililowasilishwa, pamoja na kuchukua hatua.

Kwa upande wake Afisa Elimu Sekondari Janeth Moyo alisema kulingana na tathimini iliyofanyika kwa kipindi cha muhula wa kwanza wa masomo kuanzia januari 2023 hadi Mei 2023 takwimu zinaonesha ni 37% za wanafunzi wa za **Sekondari** ndio wanaopta chakula cha mchana shulenia ambapo hupelekea kuwa na matokeo yakitaaluma yasiyoridhisha.

# MKUU WA WILAYA YA SONGEA AMEWATAKA WATAALAMU KUKAMILISHA MIRADI YA BOOST KWA WAKATI



Mkuu wa Wilaya ya Songea Kapenjama Ndile amewataka Walimu wa kuu na Maafisa watendaji kusimamia miradi ya BOOST ambayo na kuhakikisha inakamilika ifikapo juni 30 2023 ambayo inajengwa katika shule saba 7 za Msingi kwa lengo la kuboresha miundo mbinu ya kusomea na kujifunzia ya Elimu Msingi na awali





Hayo yamejili katika ziara ya Mkuu wa Wilaya iliyofanyika kwa siku moja kwa lengo la kukagua hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya BOOST ambayo inatekelezwa katika shule ya msingi Kipera, Shule ya Msingi Mbulani, Shule ya Msingi Ruhuwiko, Shule ya Msingi Matogoro, Shule ya Msingi Mkuzo, Shule ya Msingi Amani, Shule ya Msingi Bombambili.

Mhe. Ndile alisema Manispaa ya Songea imepokea Mil. 893 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo ikiwemo na ujenzi wa shule mpya hivyo amewataka wataalamu hao kuwajibika ipasavyo ili kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati.

# BIL. 4 ZAJENGA VITUO VYA AFYA MANISPAA YA SONGEA





Mstahiki Meya Manispaa ya Songea Michael Mbano amefanya ziara ya kutembelea miradi ya afya inayoendelea kujengwa katika kata ya Tanga, Lilambo, pamoja na kata ya Mletele. Ziara hiyo imefanyika kwa siku tatu 3 kuanzia tarehe 06 juni 2023 hadi 08 Juni 2023 ambapo alifanikiwa **kutembelea** kituo cha afya Lilambo kilichoojengwa kwa thamani ya Mil. 550 fedha za mapato ya ndani na kimeanza kutoa huduma za awali, Kituo cha afya Mletele kinachojengwa kwa thamani ya Mil. 545 fedha kutoka Global Fund, pamoja na ujenzi wa Hospital ya






Manispaa ya Songea inayojengwa kwa thamani ya Bil. 1 fedha kutoka Serikali kuu.
Mhe. Mbano "ametoa shukrani kwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha kiasi cha Bil 4 kwa lengo la kupunguza kero ya umbali wa upatikanaji wa huduma za Afya."



Aliongeza kuwa, kituo cha afya Mletele kimegharimu jumla ya kiasi cha fedha Mil. 845 fedha ambazo Mil 545 zimetumika kwajili ya ujenzi na Mil 300 kwa ajili ya vifaa tiba ambapo ujenzi utakamilika mara ifikapo tarehe 30 juni 2023.

# YALIYOJIRI SIKU YA KIMATAIFA YA UELEWA KUHUSU ALBINO.



Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Serikali ilitenga bajeti ya shilingi Mil. 50 kwa ajili ya kuboresha huduma za utoaji wa mafuta kinga kwa watu wenye ualbino nchini.

Utekelezaji wa huduma mbalimbali nchini umezingatia Sera, Mikataba ya kikanda, na kimataifa na Mipango mbalimbali ya nchi ikiwemo na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Sera ya Taifa ya huduma na maendeleo kwa watu wenye ulemavu, sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mwaka 2010, na Mkataba wa Kimataifa wa watu wenye ulemavu 2006.

Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza Halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kinga pamoja na kuongeza wataalamu kwa lengo la kudhibiti saratani ya ngozi kwa watu wenye Ualbino.

Hayo yamejili katika kuadhimisha kilele cha Siku ya Kimataifa ya uelewa kuhusu Albino iliyofanyika kuanzia tarehe 11 juni hadi 13 juni 2023 Mkoani Ruvuma katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na viongozi wa kitaifa pamoja na wadau mbalimbali kwa lengo la kutoa uelewa kuhusu Albino.

Mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kazi, Vijana,Ajira na Wenye Ulemavu Prof Joyce Ndalichako (MB) ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban Thomas.

Akizungumza Mkuu wa Wilaya ya Songea Wilman Kapenjama Ndile kwaniaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma " Amewataka Maafisa Ustawi wa Jamii kuhakikisha wanapata takwimu sahihi kwenye maeneo yao za watu wenye Ualbino kwa ajili ya kutoa huduma muhimu."

Ndile aliongeza kuwa, katika kuimarisha juhudi mbalimbali za ustawi wa jamii kwa watu wenye ulemavu Serikali imechukua hatua za kuwawezesha walemavu kiuchumi pia kwa kutambua juhudi za Serikali katika kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. *"Alibainisha"*

" Serikali inachukua hatua mbalimbali katika kutekeleza matakwa ya kisheria ya watu wenye ulemavu kwa kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025."



Amewataka kuushirikiano, kujenga upendo na kufanya kazi kwa pamoja ili kuepuka migogoro inayoweza kuleta chuki au kusambaratisha umoja na kuendelea kuchangamkia fursa adhimu ili kujikwamua kiuchumi kwa kufanya marejesho ya mikopo ili kutoa fursa kwa wengine waweze kunufaika.



Kwa upande wake Mwenyekiti wa Vyama vya Walemavu Tanzania ( SHIVYAWATA) Ernest Simaya alisema “ Maadhimisho hayo yalianza mwaka 2006 na hatimaye kuungwa mkono na Mataifa  mbalimbali. Ajira kwa watu wenye ulemavu imesimamia Takwa la 3% kuajiri  watu wasiopungua  20 ambapo katika kipindi cha mwaka 2023 Serikali imeajiri watumishi 812 na Intenalship 178.





Simaya alisema mambo ya msingi ambayo huyashughulikia ni pamoja na suala la ajira kwa walemavu ambapo kwa mwaka 2021/2022 Serikali imeajiri watumishi walimu ( walemavu) 245. “***Alibainisha.”***

# MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

Maadhimisho siku ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 16 Juni kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ikiwemo Nchi ya Tanzania ambapo chimbuko la maadhimisho hayo ni baada ya kutokea kwa mauaji ya watoto 2000 yaliyofanywa na Utawala wa Makaburu katika kitongoji cha SOWETO nchini Afrika ya Kusini mnamo tarehe 10 Juni 1970.

Mauaji hayo yalitokea wakati wa maandamano ya wanafunzi kwa lengo la kupinga Mfumo wa Elimu ya kibaguzi iliyokuwa inatolewa na Utawala wa Afrika ya Kusini ambapo 1991 Uongozi wa Nchi za Afrika walifanya uamuzi wa kuienzi siku hiyo ikiwa ni kumbu kumbu ya mauaji ya watoto hao.



Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Wilaya ya Songea Mhe. Elizabeth Nyembele ambayo yamefanyika kihalmshauri na kuhudhuriwa na viongozi, wadau pamoja na wanafunzi yaliyofanyika katika Uwanja wa Majimaji leo tarehe 16 Juni 2023.

Bi Elizabeth amesema Serikali imeridhia na kusaini Mikataba inayohusu Haki za Watoto (1991) na Mkataba wa Afrika wa Haki ya Ustawi wa Mtoto ya mwaka 2005 ambayo yote kwa pamoja imetoa miongozo ya kusimamia ulinzi na haki kwa mtoto.

Katika kuimarisha ulinzi wa mtoto Manispaa ya Songea kupitia jeshi la polisi imeanzisha dawati la jinsia na watoto katika kituo cha Polisi kwa lengo la kupokea taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto na watuhumiwa kuchukuliwa hatua za kishera pamoja na uundaji wa kamati za ulinzi wa mwanamke ngazi ya Wilaya, kata na mitaa kwa lengo kuibua changamoto na namna ya kuzitatua.
**"Alibainisha**".

"Ametoa wito kwa wazazi au walezi wahakikishe wanawasimamia watoto nakujiepusha kwenda kwenye maeneo ambayo ni hatari kwa usalama, kufuatilia mienendo na kumuepusha mtoto na vitendo vya ukatili ikiwa pamoja ulawiti na mimba, ubakaji, matumizi mabaya ya mitandao na simu, pamoja na kutoa malezi yenye maadili na kutimiza wajibu wa kuheshimu wazazi, walimu na jamii."

Kwa upande wake Mratibu wa Maadhimisho (Afisa Maendeleo ya Jamii ) Bi Joyce Mwanja alisema "Kauli mbiu ya mwaka 2023 inaelekeza kuweka mazingira Salama na kuchukua tahadhari dhidi ya watoto wanapokuwa mitandaoni ambayo inaikumbusha jamii pamoja na wazazi kutumia matumizi sahihi na salama dhidi ya vifaa vya kieletroniki na intanenti kutokana na uwepo wa vitendo vingi vya ukatili vinavyofanyika mitandaoni ikiwemo na simu.

Bi Joyce aliongeza kuwa kauli mbiu hiyo imelenga kuhamasisha Serikali, Wananchi, Taasis, Asasi, wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika suala la malezi, makuzi, ulinzi na maendeleo ya mtoto.

# RC RUVUMA AIPONGEZA MANISPAA YA SONGEA KUPATA HATI SAFI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban Thomas ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa kupata Hati ya Kuridhisha ya Hoja ya Ukaguzi katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo ambayo imetokana na uwajibikaji na usimamizi wa wataalamu katika kujibu hoja za ukaguzi wa hesabu za Serikali.

Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Manispaa ya Songea ilipata Hati inayoridhisha, mwaka 2020/2021 Manispaa ya Songea ilipata Hati inayoridhisha na mwaka 2021/2022 Manispaa ya Songea imepata Hati inayoridhisha.

Hayo yamejili katika Baraza la Hoja za Ukaguzi lililofanyika **tarehe** 22 Juni katika ukumbi wa Manispaa ya Songea ambayo imehudhuriwa na Madiwani, Wataalamu mbalimbali, viongozi ngazi ya Mkoa na Wilaya katika ukumbi wa **Masnispaa** ya Songea kwa lengo la kupokea taarifa za ya utekelezaji wa mapendekezo ya mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
Amewataka Wataalamu kuhakikisha wanatoa ushirikiano katika kujibu Hoja zote Ukaguzi kwa wakati na kuzipatia utatuzi.

Kanal. Laban ametoa wito kwa Waheshimiwa Madiwani, Maafisa watendaji wa kata na mitaa wahakikishe wanasimamia Miradi ya Maendeleo ambayo inatekelezwa na Halmashauri pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato.

Ametoa Rai kwa wataalamu kuhakikisha wanafuatilia madeni ya vikundi vyote ambavyo vinadaiwa ili waweze kurejesha mikopo na hatimaye kutoa furusa kwa wanavikundi wengine.
Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma Komredi Oddo Mwisho ametoa pongezi kwa kupata Hati inayoridhisha pamoja na Uwajibikaji wa viongozi katika kusimamia Miradi ya Maendeleo ambayo inaendelea kujengwa. **"Alipongeza."**

Mkuu wa Wilaya ya Songea Wilman Kapenjama Ndile amesema Ukuaji wa Uchumi katika Sekta ya madini umepelekea ukuaji wa pato la Taifa ambapo Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa mitatu ambayo inaongoza katika uchangiaji wa pato la Taifa kupitia madini.

Kwa upande wake Mstahiki Meya Manispaa ya Songea Michael Mbano amewataka Madiwani, na Wataalamu wahakikishe wanasimamia ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo la 100% lililowekwa na Halmshauri pia kuhakikisha wanatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

# TAPSHA YAWATAKA WALIMU KUONGEZA UWAJIBIKAJI



Umoja wa Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania TAPSHA " Tanzania Primary School Head Teachers Association ambao umesajiliwa na kutambulika kisheria ambapo uliundwa kwa lengo la kuwaunganisha walimu wakuu wote ngazi ya Halmashauri, Mkoa hadi ngazi ya Taifa.

TAPSHA Manispaa ya Songea ina jumla ya wanachama 92 kati yao shule 81 ni za Serikali na 11 ni shule binafsi ambapo kupitia umoja huo wameweza kufanikisha kutatua changamoto mbalimbali kwa kushirikiana na viongozi ngazi ya Halmshauri ambao umepelekea kufanya vizuri kitaifa na kuzawadiwa cheti cha pongezi kwa Afisa Elimu Manispaa ya Songea kwa malezi bora ya walimu hao.

Hayo yamejili katika kikao kazi cha mwaka kilichofanyika leo 21 juni 2023 katika ukumbi wa SACOS ya Walimu kilichohudhuriwa na viongozi kutoka Halmashauri, Wanachama na Wadau wa Elimu kwa lengo la kufanya tahimini na kuboresha Taaluma katika Manispaa ya Songea.

Akizungumza Afisa Elimu Manispaa ya Songea Frank Sichalwe "amewataka wakuu wa shule wote kuongeza uwajibikaji na kubaini changamoto za kitaaluma na namna ya kuzitafutia ufumbuzi ili kuleta mabadiliko chanya ya ufaulu kwa wanafunzi." ***Alisisitiza***



Naye Menyekiti wa TAPSHA Manispaa ya Songea Mwl. Siwetu Ahamadi amesema TAPSHA imejiwekea mikakati ambayo itawezesha kuinua hali ya ufaulu kwa wanafunzi ikiwemo na kuendelea kusimamia na kuandaa mitihani ya upimaji "pre-National kwa madarasa yenye mitihani ikiwemo na darasa la saba, na darasa la nne.

Kwa upunde wa Walimu wakuu waliohudhuria kikao hicho wamesema umoja huo unawasaidia katika kubadilishana uzoefu katika utendaji wa kazi na kuwaweka karibu. " ***wameshukuru"***

# YALIYOJIRI SIKU YA WAJANE DUNIANII

Siku ya Wajane Duniani huadhimishwa kila ifikapo tarehe 23 Juni kila mwaka baada ya Umoja wa Mataifa kupitisha siku hii kuwa ya kimataifa kupitia Azimio Na. A/RES/65/189 la tarehe 21 Desemba 2010 na ilianzishwa na kuasisiwa na Lord Loomba mwaka 2005.
Kutokana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wajane wanachama wa Umoja wa kimataifa waliazimia kuadhimisha siku hii kwa lengo la kuongeza uhamasishaji wa kupinga ukiukaji wa haki za binadamu kwa wajane.




Akizungumza Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Ruvuma Xsaveria A.Mlimira amewataka maafisa ustawi wa jamii na maafisa watendaji kata/mitaa kuendelea kuelimisha jamii juu ya uga-waji wa mirathi kuzingatia kanuni na sheria ili kuleta usawa na haki ikiwemo haki ya kuwalea watoto, haki ya kumiliki Ardhi pamoja na mali.
Hayo yamejili katika kilele cha maadhimisho ya siku ya wajane Duniani ambayo yamefanyika tarehe 23 Juni katika ukumbi wa Manispaa ya Songea kuudhuriwa na viongozi wa Dini, Watalaamu pamoja na wananchi ambapo yakiwa na lengo la kuimarisha ushirikiano na kutatua changamoto katika jamii.

**Kupitia sanse ya watu na makazi ya mwaka 2023 Tanzania ina jumla ya wajane 1,396,262 ambapo serikali imefanikiwa kutatua changamoto mbalimbali ikiwemo kuanzishwa kwa kampeni ya "maadili yetu Taifa letu" kwa lengo la kuwatunza na kuwalinda wajane, kuanzishwa madawati ya jinsia na watoto 573 katika vituo vya Jeshi la Polisi na Magereza kwa lengo la kutokomeza ukatili wa kijinsia wakiwemo wajane pamoja na kuundwa kwa Wizara mahsusi ya Maendeleo ya Jamii,jinsia,wanawake na makundi maalum.***Alisema.*

Kwa upande wake Afisa Dawati la jinsia na watoto Songea Sajenti Paulina ametoa rai kwa wajane kutoa taarifa kwa wakati ili kupata msaada wa kisheria pale ambapo wanakutana na changamoto ikiwemo kunyanyashwa na kunyimwa haki ya umiliki wa mali.

Wametoa shukrani za dhati kwa serikali ya awamu ya sita kwa kuwatambua na kuwajali wajane kwa kuweka mifumo ya kulinda haki na kuongeza huduma za msaada wa kisheria Na: 1ya mwaka 2017.***Wananchi Walishukuru***

# MKUU WA MKOA WA RUVUMA AMEZITAKA NGO'S KUTOA TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban Thomas amezitaka NGO'S (Mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha wanaweka uwazi wa taarifa ya mapato na matumizi katika shughuli zote **zinazotekelezwa** katika Halmashauri na Mikoa ili kuondoa malalamiko na kujenga imani katika jamii.

Hayo yamebainishwa tarehe 28 Juni 2023 katika kikao kazi cha tathimini ya utekelezaji wa shughuli za Mashirika yasiyo ya Kiserikali Mkoa wa Ruvuma kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na wadau wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali pamoja na viongozi ngazi za Wilaya na Mkoa kwa lengo la kuona mafanikio na changamoto wanazokutana nazo pamoja na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2022/23.

Kanal. Laban alisema ni wajibu wa NGO'S kuandaa bajeti ya vikao pamoja na kushiriki matukio ya kitaifa ikiwemo na Siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Familia, Siku ya Ukimwi Duniani, ili kuleta ushirikishwaji katika jamii.

"Amewataka Mashirika yasiyo ya Kiserikali Mkoani Ruvuma kuhakikisha wanalipa stahiki za watoa huduma na wasimamizi wote katika Halimashauri kwa wakati ili kuondoa malalamiko pamoja na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa msajili ngazi ya Halmashauri na Mkoa



Kwa upande wake Msajili Msaidizi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Mkoa wa Ruvuma Xsaveria Mlimira alisema Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali 166 ambayo yanajishughulisha na sekta mbalimbali za maendeleo ikiwemo na Afya, Elimu Kilimo na nyinginezo.

Mlimila alisema Miongoni mwa mafanikio katika Sekta ya Afya katika eneo la UKIMWI hadi kufikia Machi 2023 katika 95 ya kwanza Mkoa umefikia 113,1%, ya Pili Mkoa umefikia 98.3%, na ya tatu 95.9%.

Mafanikio katika Sekta ya kilimo kuanzia mwaka 2019 hadi 2023 zaidi ya wakulima wadogo 10,000 kwenye vikundi zaidi ya 300, katika vijiji 205 kwenye kwenye kata 60 za Halmashauri 6 katika Mkoa wa Ruvuma wamefikiwa moja kwa moja na huduma zinaendelea kutolewa.

# RC RUVUMA KANAL. LABAN THOMAS, ARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI MRADI WA BOOST



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Laban Thomas ametoa pongezi kwa Wataalamu wa Manispaa ya Songea kwa usimazi na ufuatiliaji mzuri wa Miradi ya Maendeleo inayoendelea kutekelzwa kupitia Mradi wa Boost ambayo ipo katika hatua ya Ukamilishaji.

Manispaa ya Songea imepokea fedha kutoka Serikali kuu kupitia mradi wa kuboresha upatikanaji wa fursa sawa katika ujifunzaji bora wa elimu ya awali na Msingi Tanzania Bara (BOOST) kiasi cha Shilingi mill. 893 kwa ajili ya ujenzi wa shule 7 za Msingi ambazo ni Kipera, Amani, Matogoro, Bombambili, Mkuzo na Ruhuwiko ambayo ilianza ujenzi tarehe 15 Mei 2023).

Kanal Laban alisema" Ameridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi wa madarasa , Vyoo na majengo ya utawala ambapo amewataka wataalamu kuendelea kuwasimamia mafundi ili wawewze kukamilisha ujenzi kwa wakati ili majengo hayo yaweze kutumika na wanafunzi mara baada ya kufunguliwa shule."

"Amewataka walimu kuhakikisha wanaboresha mazingira ya shule kwa kupanda miti ya vivuri, pamoja na maua ili kuweka mazingira safi na kuachana na kutumia fagio mara kwa mara kwa ajili ya kufagia mazingira badala yake waweke bustani ya maua**."** **Alisisitiza."**

Hayo yamejiri wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanal. Lban Thomas kwa lengo la kukagua miradi iliyofanyika tarehe 28 Juni 2023 katika Manispaa ya Songea ambapo alitembelea Shule ya Msingi Kipera ambayo ilipokea Fedha Mil. 513 kwa ajili ya Ujenzi wa Madarasa 16, matundu ya vyoo 24,na jengo la utawala pamoja na shule ya Msingi Ruhuwiko ambayo ilipokea fedha Mil 77 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 3 na matundu ya vyoo 3.
Ametoa Rai kwa viongozi wa Serikali za Mitaa kuwashirikisha wananchi wakati wa utekelezaji wa miradi ili kujenga ushirikiano katika kulinda mazingira pamoja na miundombinu ya shule.
Alitoa Pongezi kwa Serikali ya awamu ya Sita



inaongozwa na Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha Mil 893 kupitia Mradi wa BOOST ili kuboresha miundombinu ya Elimu ya awali na Msingi**.**

Wananchi wakitoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, ambapo walisema mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa madarasa hayo yataondoa chagamoto ya mlundikano wa Wanafunzi darasani **.**

# KWA HABARI ZAIDI

www.songeamc.go.tz

Songea MC

SONGEA ONLINE TV